# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## IDARA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

# MPANGO WA TAIFA WA KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAAFA 2022

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# IDARA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

# MPANGO WA TAIFA WA KUJIANDAA NA KUKABILIANA NA MAAFA 2022

## DIBAJI



Tanzania Bara ipo katika hatari ya kuathirika na majanga ya asili na yale yanayosababishwa na shughuli za binadamu ambayo yanahatarisha na kuathiri maisha ya watu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ni muhimu kutambua na kuelewa chanzo cha majanga na kuandaa mpango wa kujiandaa na kukabiliana na maafa ambao utahusisha wadau mbalimbali. Serikali iliandaa Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa Tanzania (TEPRP) mwaka 2012 ili kuhakikisha wadau wanajiandaa kuchukua hatua za haraka kabla na wakati wa maafa. Hata hivyo, maendeleo ya kiteknolojia na maarifa mapya yanayoibuka katika usimamizi wa maafa yamechangia kuleta msukumo kwa Serikali kufanya mapitio ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2012. Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa uliofanyiwa mapitio wa mwaka 2022 unatoa miongozo ya uratibu wa majukumu na kazi za wadau zitakazotekelezwa kushughulikia maafa yanayotokana na aina zote za majanga.

Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa ni mpango kazi wa kushughulikia majanga mbalimbali ambao unaweka hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana maafa. Mpango unalenga kuwezesha uratibu wa utoaji wa rasilimali na huduma muhimu ili kukabiliana na matukio ya maafa. Aidha, Mpango huu unaelezea hali ya maafa na mipango inayotarajiwa, dhana ya uendeshaji, hatua za kukabili na kurejesha hali, majukumu na shughuli mahususi katika kukabili maafa kwa Wizara, Idara na Taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali. Mpango huu unazingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Sura 242.

Maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022 yamezingatia hali ya sasa ya maafa nchini, mifumo ya kitaasisi, mahitaji na maendeleo katika shughuli za kujiandaa na

kukabiliana na maafa kimataifa. Majukumu mbalimbali kuhusu kujiandaa na kukabiliana na maafa yameboreshwa kwa kuzingatia uzoefu, mwenendo wa madhara ya maafa na mtazamo wa Serikali katika ustahimilivu wa maendeleo. Mapitio haya yamefanyika kwa lengo la kuimarisha uwezo wa taasisi za umma na wadau wengine katika kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Mpango unawezesha uratibu wa kimfumo wa utekelezaji wa shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa, kwa kuzingatia taasisi yenye jukumu la msingi kwa mujibu wa sheria. Aidha, mpango umezingatia ushirikiano wa sekta nyingine na taasisi zisizo za kiserikali ili kuhakikisha mahitaji na huduma wakati wa maafa yanashughulikiwa kikamilifu katika mtazamo wa uwajibikaji wa pamoja. Hivyo, nasisitiza wadau kujiandaa wakati wote kwa kuwa na wataalam, vifaa, misaada ya kibinadamu na kuwa wabunifu ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa majukumu yaliyoainishwa katika mpango huu ili kuokoa maisha ya watu na mali zao kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii.

Kassim Majaliwa Majaliwa (MB.)
**WAZIRI MKUU**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## SHUKRANI




Maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022 yamefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao walitoa michango yao. Maoni yaliyotolewa na wadau yamesaidia katika kufafanua majukumu na wajibu wa taasisi zinazohusika na shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa nchini.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara na Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi za Taaluma na Utafiti, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Vyombo vya Habari na Sekta Binafsi kwa kushiriki kikamilifu katika kutoa michango yao ambayo imewezesha kufanikisha maandalizi ya mpango huu.

Natoa shukrani za dhati kwa Benki ya Dunia kwa msaada wa kifedha na kitaalamu uliotolewa kupitia taasisi ya *Earthquakes and Megacities Initiative (EMI)*. Aidha, ninatambua msaada wa kifedha kutoka Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) uliowezesha maandalizi ya mwisho ya mpango huu kupitia Jukwaa la Taifa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa.

Ni matarajio yangu kuwa ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali utaendelea wakati wa utekelezaji wa mpango huu.



Dkt. John A. K. Jingu
**KATIBU MKUU**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**(SERA, BUNGE NA URATIBU)**

# YALIYOMO


DIBAJI ........ I

SHUKRANI ........ III

UTANGULIZI........III

UFAFANUZI WA MSAMIATI ........ VIII

SEHEMU YA KWANZA: MPANGO MKUU ........ 1

1. UTANGULIZI ........ 1

MAMLAKA ........ 3

A. MIONGOZO YA KISHERIA ........ 3

B. SHERIA ZA KISEKATA KUHUSU USIMAMIZI WA MAAFA NCHINI TANZANIA ........ 3

C. SERA YA TAIFA YA MENEJIMENTI YA MAAFA YA MWAKA 2004 ... 4

D. MPANGILIO WA KITAASISI WA USIMAMIZI WA MAAFA TANZANIA BARA ........ 4

2. LENGO ........ 5

3. UPEO ........ 3

4. HALI HALISI ........ 7

I. WASIFU WA NCHI ........ 7

A. MAMBO YANAYOCHANGIA KATIKA UWEZEKANO WA KUATHIRIKA ........ 8

B. MAJANGA YANAZOWEZA KUTOKEA NCHINI ........ 9

C. UCHAMBUZI WA HATARI YA MAAFA ........ 15

5. MIPANGO TARAJIWA ........ 16

6. DHANA YA KUKABILI ........ 17

7. MUUNDO NA MGAWANYO WA MAJUKUMU ........ 19

A. MUUNDO ........ 19

B. MGAWANYO WA MAJUKUMU ........ 19

8. MAJUKUMU YA KONGANI........ 21

9. MAANDALIZI NA MAPITIO YA MPANGO ........ 36

SEHEMU YA PILI: VIAMBATISHO ........ 37

KIAMBATISHO A: SAA 72 ZA KWANZA ZA MAAFA ........ 37

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Muhtasari wa majanga makubwa nchini ..................... 10
Jedwali Na. 2: Bangokitita la Tathmini ya Uchambuzi wa Hatari nchini ........................................................................................................ 15
Jedwali Na. 3: Taratibu za Kiutendaji kwa kila Kongani- Wadau, Maelezo na Kazi ........................................................................ 21

## VIELELEZO

Kielelezo **Na. 1**: Muundo wa usimamizi wa maafa nchini ................. 5

# UFAFANUZI WA MSAMIATI

| | |
|---|---|
| Janga | Maana yake ni balaa au baa linalotokana na nguvu za asili au shughuli za kibinadamu ambalo linaweza kusababisha maafa. |
| Kujiandaa na Maafa | Ni shughuli zinazofanyika katika kulinda uhai wa binadamu na mali pamoja na viashirio visivyoweza kudhibitiwa kwa hatua za kawaida za upunguzaji maafa. Hivyo, shughuli za kujiandaa na maafa hufanyika katika sehemu ambapo madhara ya maafa yatatokea na kwamba mipango, hatua na rasilimali za uokoaji zinapaswa kuandaliwa kabla ya tukio. Hii hufanyika siyo tu kuhimiza utayari wa haraka na wa uhakika kwa matishio au madhara makubwa yanayoweza kutokea, bali pia kuongoza katika hatua ya urejeshaji hali baada ya maafa. |
| Kukabiliana na maafa | maana yake ni hatua yoyote inayochukuliwa mara tu baada ya maafa kutokea ili kuokoa maisha, mali na mazingira, kupunguza madhara ya kiafya, kutoa huduma za kibinadamu, kuimarisha usalama wa umma au kushughulikia uharibifu unaotokana na maafa. |
| Kupunguza madhara | Maana yake ni hatua zinazoelekezwa katika kupunguza madhara ya maafa yanayoweza kusababishwa na tukio la janga. |
| Kurejesha hali baada ya maafa | Maana yake ni hatua zinazosaidia kurejesha hali au kuboresha mifumo ya maisha iliyoathiriwa na maafa kwa kujenga upya au kurejesha mifumo kwa ubora zaidi ili kuzuia au kupunguza madhara ya maafa siku zijazo. |
| Kuzuia maafa | Maana yake ni hatua zinazochukuliwa kuzuia hatari mpya au kupunguza hatari zilizopo kutokana na shughuli na maamuzi ya kibinadamu au nguvu za asili yasisababishe kutokea kwa maafa. |
| Maafa | Maana yake ni madhara yanayotokana na janga ambayo yanajumuisha uharibifu wa mfumo wa kawaida katika jamii, kusababisha vifo, majeruhi, madhara ya kisaikolojia, upotevu au uharibifu wa mali, mifumo mbalimbali ya kiteknolojia na huduma za kiuchumi na kijamii au mazingira kwa kiwango chochote ambapo jamii iliyoathirika haiwezi kukabili kwa kutumia rasilimali zake bila msaada kutoka nje ya jamii hiyo. |
| Makundi maalum | Maana yake ni makundi yanayojumuisha watoto, wanawake wajawazito, wazee, watu wenye ulemavu, watu wenye utapiamlo, wakimbizi, wahamiaji wa ndani |

| | |
|---|---|
| | na wagonjwa au wenye upungufu wa kinga. |
| Mkakati wa Taifa wa Uratibu na Udhibiti wa hatari za maafa | Maana yake ni mkakati ambao unaainisha hatua zitakazochukuliwa katika kuzuia na kupunguza madhara ya majanga pamoja na kujiandaa kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea. |
| Kituo cha Kukabili Dharura | Ni nyezo timilifu na mahususi ambayo hutumiwa na maofisa wa Serikali katika kuelekeza na kudhibiti na kuratibu rasilimali muhimu katika kipindi cha dharura |
| Usimamizi/Menejimenti ya Maafa | Ni usimamizi wa rasilimali na majukumu ya kushughulikia masuala yote ya maafa hususan kujiandaa, kukabili na hatua za awali za urejeshaji. |
| Uratibu na udhibiti wa hatari za maafa (Uratibu na uratibu na udhibiti wa hatari za maafa) | Maana yake ni utekelezaji wa sera na mikakati ya kupunguza hatari za maafa ili kuzuia hatari mpya, kupunguza hatari zilizopo na kudhibiti hatari zilizobaki kwa lengo la kuimarisha ustahimilivu na kupunguza hasara za maafa. |

## SEHEMU YA KWANZA: MPANGO MKUU

### 1. UTANGULIZI

A. Mpango huu unaainisha hatua za kuchukuliwa na Taasisi za Serikali, Taasisi za Umoja wa Mataifa, Taasisi za Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Kujitolea na wadau wa menejimenti ya maafa ili:

(i) Kuzuia maafa na kupunguza uwezekano wa kuathirika kwa jamii pale maafa yoyote yanapotokea.

(ii) Kuanzisha uwezo wa kuilinda jamii dhidi ya madhara ya maafa.

(iii) Kuitikia kwa haraka dhidi ya matukio yoyote ya maafa yanayotokea na kuleta athari kubwa ndani ya nchi.

(iv) Kupanga kurejesha hali baada ya maafa au dharura kutokea.

B. Mpango huu hautajihusisha na matukio yanayotokea kila siku, ambayo hayasababishi matatizo makubwa na hushughulikiwa na idara na wakala za Serikali kila wakati. Mpango unalenga kushughulikia maafa makubwa yanayohitaji mahitaji na kusababisha maumivu ambayo waathirika hawawezi kuyaepuka bila msaada, na yanayohitaji matumizi makubwa ya rasilimali za taifa.

C. Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa ni mpango tekelezi wa majanga ambao:

(i) Utakaotumiwa na Serikali katika shughuli za usimamizi wa maafa.

(ii) Viambatisho ambavyo vinafafanua shughuli mahususi na muhimu za kujiandaa na kukabilina maafa.

D. Mpango huu unapaswa kueleweka miongoni mwa wadau wote muhimu ambao watautekeleza vizuri vinginevyo hautatekelezeka. Hivyo basi, maofisa wanaohusika wa Serikali, wakuu wa idara na wakala na taasisi za kujitolea watatakiwa kuelewa majukumu yao na wajibu katika matukio ya maafa.

E. Mpango huu unabadilika na wakati. Majanga mapya hutokea, hali hubadilika, sheria zinaweza kubadilika, sera zinaweza kupitiwa, wizara za Serikali zinaweza kubadilishwa. Hivyo, mpango unahitaji kupitiwa na kuboreshwa kila kipindi ili kujumuisha mabadiliko haya. Kwa kushirikiana na Idara ya Menejimenti ya Maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, idara zote, wakala, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na majukumu waliyopewa watawajibika kupitia na kuboresha sehemu zao wanazohusika katika mpango. Watapitia na kuboresha maeneo yao ndani ya mpango kama itakavyohitajika kufuatana na uzoefu katika maafa, upungufu uliobainika katika mafunzo na mazoezi na mabadiliko katika mfumo wa Serikali na taasisi zinazojishughulisha na dharura.

F. Mpango huu unapotumiwa ipasavyo na kusasishwa mara kwa mara unaweza kusaidia maafisa wa serikali katika kujiandaa na kukabiliana vilivyo na majanga ya asili na yale yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu na kuwalinda wananchi dhidi ya athari za matukio haya.

## MAMLAKA

**A. Miongozo ya Kisheria**

Mpango wa Taifa wa kujiandaa na Kukabiliana na Maafa umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya kisheria ifuatayo: -

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), ambayo inampa Rais mamlaka ya kutangaza hali ya dharura iwapo kuna tukio kubwa la maafa linalotishia taifa;

(ii) Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na.6 ya Mwaka 2022 ambayo inaipa Mamlaka Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa kuandaa mipango ya kusimamia maafa nchini.

**B. Sheria za kisekta kuhusu usimamizi wa maafa nchini**

Matukio ya majanga yanayotokana na nguvu za asili na shughuli za kibinadamu hushughulikiwa na sekta tofauti. Kadhalika, usimamizi madhubuti wa hatari za maafa unahitaji matumizi ya Sheria za Sekta mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya udhibiti wa maafa. Sheria hizi ni pamoja na:

| NA. | SHERIA | SURA |
|---|---|---|
| 1. | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira | 191 |
| 2. | Sheria ya Magonjwa ya Wanyama | 156 |
| 3. | Sheria ya Nishati ya Atomiki | 188 |
| 4. | Sheria ya Usafiri wa Anga | 80 |
| 5. | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira | 191 |
| 6. | Sheria ya Nguvu za Atomiki | 45 |
| 7. | Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji | 427 |
| 8. | Sheria ya Usalama wa Chakula | 249 |
| 9. | Sheria ya Madini | 123 |
| 10. | Sheria ya Afya na Usalama Kazini | 297 |
| 11. | Sheria ya Petroli | 392 |
| 12. | Sheria ya Afya ya Mimea | 133 |
| 13. | Sheria ya Bandari | 166 |
| 14. | Sheria ya Reli | 170 |
| 15. | Sheria ya Ardhi | 113 |

| | | |
|---|---|---|
| 16. | Sheria ya Usafiri wa Majini ndani ya Nchi | 172 |
| 17. | Sheria ya Trafiki Barabarani | 168 |
| 18. | Sheria ya Mipango ya Nchi na Miji | 378 |
| 19. | Sheria ya Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Viwanda Tanzania | 176 |
| 20. | Sheria ya Mifugo | 319 |
| 21. | Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira | 272 |

**C. Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004**

Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 inatoa maelekezo ya kisera yenye lengo la jumla la kufanya kazi kwa mfumo madhubuti na wenye tija wa kudhibiti maafa utakaopunguza athari mbalimbali ikiwemo kupoteza maisha, uharibifu wa mali na mazingira Tanzania Bara.


**D. Mpangilio wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Maafa Tanzania Bara**

Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Menejimenti ya Maafa ndiyo yenye jukumu la kuratibu shughuli zote za udhibiti wa maafa nchini. Idara inaratibu shughuli za kuzuia na kujiandaa kukabiliana na maafa ili kupunguza athari za maafa kwa jamii na mali zao pamoja na mazingira. Muundo wa uratibu unatoa majukumu ya msingi ya usimamizi wa hatari za maafa na utoaji wa misaada na huduma za kibinadamu kutoka katika sekta zote na wadau mbalimbali walioidhinishwa kisheria ikiwa ni pamoja na Wizara, Taasisi za Umma, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Wadau wa Maendeleo.

Mfumo wa Usimamizi wa Maafa nchini umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni upande wa maamuzi na utendaji. Upande wa maamuzi kuna Kamati Elekezi za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Upande wa utendaji ni kupitia Kamati za Kitaalam za Usimaimzi wa Maafa za Taifa, Mkoa na Wilaya. Upande utendaji una jukumu la kuchambua na kupendekeza hatua za kitaalam

kwa watoa maamuzi ili waweze kutekeleza majukumu yao. Kamati za kitaalam zinaweza kuunda kamati ndogo mbalimbali za wataalam kama vile kikosi maalum au vikundi vya kazi vya kiufundi katika kurahisiaha utekelezaji wa majukumu yake. Katika ngazi Kata na Kijiji/Mtaa kuna Kamati za Usimamizi wa Maafa ambazo hutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa kwenye maeneo yao. Utekelezaji wa shughuli za Kamati umezingatia umuhimu wa kukabidhi majukumu kwa Kamati ya juu iwapo kutatokea kuzidiwa na madhara ya maafa kulingana na rasilimali zilizopo au kuhusishwa kwa Kamati mbili au zaidi zilizopo katika ngazi moja. Muhtasari wa Mfumo wa kitaasisi wa menejimenti ya maafa nchini ni kama unavyoonekana katika Kielelezo Na. 1.

**Kielelezo Na. 1**: Muundo wa usimamizi wa maafa nchini




**Chanzo**: Ofisi ya Waziri Mkuu

## 2. LENGO

A. Mpango huu unaweka taratibu na miongozo ya uendeshaji ambayo itaiwezesha Serikali kuokoa Maisha ya watu, kupunguza madhara,

kulinda mali na kuhifadhi mazingira hivyo kuiwezesha Serikali kukabiliana na majanga ya asili, majanga ya kibinadamu na mabadiliko ya kiteknolojia.

B. Mpango huu unaweka miongozo ya kufanya uratibu wa shughuli za menejimenti ya maafa kwa weledi na ufanisi zaidi.

C. Mpango huu unaelezea majukumu ya wizara, idara na taasisi mbalimbali jinsi ya kujiandaa na kukabiliana na maafa na hutoa miongozo kwa kongani kumi na tano (15) zinazotekeleza shughuli za kukabiliana na maafa nchini.

D. Mpango huu unatoa mfumo mahususi wa utendaji katika kukabili maafa na unaelezea kwa undani zaidi, nani atafanya nini, kwa muda gani, na kwa namna gani.

## 3. UPEO

A. Dhana ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa inatumika kwa maafa kama ilivyofafanuliwa katika mpango huu na Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na. 6 ya Mwaka 2022, ambayo inajumuisha majanga ya asili na majanga yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu/teknolojia ambayo yatahitaji msaada wa kitaifa kukabiliana nayo.

B. Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa unashughulikia mahitaji kamili ya kibinadamu na yanayotakiwa mara kwa mara kufuatia maafa yaliyotokea; kuokoa maisha ya watu, kulinda mali, na kukidhi mahitaji ya kimsingi ya binadamu (Kujiandaa na Kukabili); na kupunguza uwezekano wa kuathirika na majanga yajayo (Kuzuia). Mpango huu haushughulikii shughuli za muda mrefu za ujenzi na za kurejesha hali.

C. Mpango huu utatumiwa na Wizara, Idara, Taasisi za Umma na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo yanaweza kupewa jukumu la kutoa usaidizi wakati wa maafa.

## 4. HALI HALISI

### I. Wasifu wa nchi

A. Tanzania Bara inaptikana katika Afrika Mashariki kati ya longitudo 29° na 41° Mashariki, na latitudo 1° na 12° Kusini. Imepakana na Bahari ya Hindi kwa upande wa Mashariki, Kenya na Uganda upande wa Kaskazini, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upande wa Magharibi, Zambia na Malawi kwa upande wa Kusini Magharibi, na Msumbiji upande wa Kusini.

B. Tanzania Bara inajumisha eneo la kilomita za mraba 945,000 ambazo kati yake, kilomita za mraba 881,000 ni nchi kavu na kilomita za mraba 61,000 za maji zinazojumuisha maziwa makuu matano (Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa na Eyasi) na vyanzo vingine vidogo vya maji ndani ya ardhi yake wakati misitu huchukua kimolita za mraba 3,000. Tanzania Bara ina ufukwe wa zaidi ya kilomita 800 kutoka Tanga hadi Mkoa wa Mtwara.

C. Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, imeonyesha idadi ya watu Tanzania Bara iliongezeka kutoka watu milioni 44.9 mwaka 2012 mpaka milioni 59.8 mwaka 2022 kwa wastani wa kiwango cha ukuaji cha asilimia 3.2

D. Miinuko ya ardhi ni kati ya mita 0-1500 juu ya usawa wa bahari na kuna maeneo makuu matatu ya fiziografia ambayo ni visiwa na uwanda wa pwani upande wa mashariki, miinuko ndani ya maji na nyanda za juu. Upande wa kaskazini na Kaskazini Mashariki, muinuko mrefu unaozaa milima ya kipekee ya volkano ambayo miongoni mwake ni Milima ya Meru na Kilimanjaro. Karibu nusu ya ardhi yote ni savanna yenye vichaka na nusu nyingine ikiwa ni nusu jangwa.

E. Bonde la ufa linaanzia Kaskazini Mashariki mwa Afrika kupitia katikati mwa Tanzania Bara na kutengeneza sehemu mbili kubwa za Bonde la Ufa Mashariki na Magharibi zinazoathiriwa na tetemeko la ardhi.

F. Tanzania Bara ina hali ya hewa ya kitropiki. Kuna misimu miwili ya mvua ambayo ni: Mvua za msimu wa msimu kati ya Desemba na Aprili na mingine miwili – yaani mvua za vuli kati ya mwezi Oktoba hadi Desemba na mvua za masika kati ya mwezi Machi na Mei. Katika msimu wa mvua za Machi-Mei hurejewa kama mvua ndefu au

'Masika' na mvua za Oktoba-Desemba kwa ujumla hujulikana kama mvua fupi au 'Vuli'.

G. Kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi na kimaisha kwa Watanzania wengi. Mwaka 2012, takriban 62.1% ya wakazi walikuwa wakulima na wanachangia takriban 25% ya Pato la Taifa (GDP). Mwaka 2016-2017, zaidi ya milioni 4.7 (40%) ya ajira za moja kwa moja milioni 11.7 na zaidi zilizotolewa kwa ajili ya Watanzania zilikuwa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Katika kiwango sawa cha kazi, kizazi hicho kilitoa huduma kwa kuzalisha takriban milioni 4.92 (42%) ya ajira zilizoundwa kwa mwaka huo (2016-2017). Kwa upande wa ajira zilizoundwa kwa kipindi hicho, Sekta za Afya na Madini zinafuata katika nafasi ya tatu na ya nne, kwa takriban 8% na 2%, mtawalia.

H. Nchi ina mabonde tisa ya mito ambayo ni Pangani, bonde la Wami/Ruvu, bonde la Rufiji, bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, bonde la ziwa Nyasa, bonde la maji ya ndani (Ziwa Eyasi, Manyara na Bubu), bonde la Ziwa Rukwa, Bonde la Ziwa Tanganyika. na bonde la Ziwa Victoria. Mito mikubwa nchini ni pamoja na Mto Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji, Malagarasi, Kagera, Songwe, Mara, Ruhuhu na Ruvuma.

## A. Mambo yanayochangia katika uwezekano wa kuathirika

Mahali: Moja ya sababu zinazochangia kuathirika, hasa katika maeneo ya pwani, ni eneo lake la kijiografia na ukaribu wa Bahari ya Hindi. Ukaribu na Bahari ya Hindi huongeza uwezekano wa kuathiriwa au kukabiliwa na hatari kama vile dhoruba za kitropiki na tsunami. Pia, eneo la makazi katika maeneo ya mitetemo au katika eneo linalokumbwa na maporomoko ya udongo au kandokando na maeneo hatarishi.

Umaskini: Kaya maskini zinakabiliwa na majanga zaidi kuliko kaya zenye kipato kikubwa. Hii ni kwa sababu kaya maskini hazina rasilimali za kutosha za kifedha kwa ajili ya kununua mahitaji na huduma muhimu kwa kutarajia tukio au baada ya maafa. Matokeo yake athari za maafa huenda zikawaathiri kwa kiasi kikubwa, ikiwa ni pamoja na kuathiriwa na viwango vya juu vya vifo.

Jinsia: Kaya zinazoongozwa na wanawake nchini zina uwezekano mkubwa wa kuwa na wakati mgumu wakati wa kukabiliana na maafa

kuliko kaya zinazoongozwa na wanaume, kutokana na ajira mahususi kwa sekta husika, kipato kidogo, upatikanaji mdogo wa pembejeo na majukumu ya malezi ya familia.

Mijini/Vijijini: Wakazi wengi wa vijijini nchini wako hatarini zaidi kutokana na kuwa na kipato cha chini na wanategemea zaidi uchumi utokanao na rasilimali za ndani kama vile kilimo, uvuvi na uchimbaji madini.

Elimu: Elimu inahusishwa na hali ya kijamii na kiuchumi, huku mafanikio ya elimu ya juu yakisababisha mapato makubwa zaidi katika jamii. Elimu ya chini inazuia uwezo wa kuelewa hatari ya maafa, taarifa za tahadhari za awali na upatikanaji wa taarifa za kukabiliana na maafa.

Makundi yenye mahitaji maalum: Makundi yenye mahitaji maalum nchini yamo katika hatari kubwa. Makundi yaliyo hatarini zaidi ni wazee, watoto, na wenye walemavu.

## B. Majanga yanazoweza kutokea nchini

Hali mbalimbali za kijiografia nchini pamoja na maendeleo ya kijamii na kiuchumi zinakabiliwa na hatari zitokanazo na majanga ya asili na yale yatokanayo na binadamu, ambazo zote zina uwezo wa kuivuruga jamii, kusababisha hasara na kuharibu mali za umma na za watu binafsi. Majanga ya asili yanayoweza kutokea ni Mafuriko, Ukame, Vimbunga, Tetemeko la Ardhi, Umeme, Maporomoko ya udongo, dhoruba, Upepo Mkali, Mmomonyoko wa fukwe za Bahari, Milipuko (Kipindupindu, Homa ya Bonde la Ufa, Mafua ya Ndege, Sumu ya Chakula, Mafua ya Nguruwe, n.k), Maambukizi ya Wadudu na Mlipuko wa Magonjwa ya Wanyama.(Kimeta, Ugonjwa wa Mdomo, Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Ngozi yenye uvimbe n.k).

Majanga yanazoweza kusababishwa na binadamu ni Mlipuko wa Moto, Ajali za Barabarani, Kuharibika kwa mifumo ya Umeme, Kuenea kwa Makazi yasiyopangwa, Uharibifu wa Mazingira na Uchafuzi wa Mazingira, Ajali za Baharini, Kuporomoka kwa Majengo, Kumwagika kwa Mafuta, Migogoro ya Kiraia, Ajali za Ndege, Nyenzo Hatarishi (pamoja na vifaa vya mionzi), Viwandani. Majanga. Muhtasari wa majanga makubwa nchini umetolewa katika **Jedwali Na. 1** hapa chini:

*Jedwali Na. 1: Muhtasari wa majanga makubwa nchini*

| Hatari | Maelezo |
|---|---|
| **Magonjwa ya mlipuko kwa wanyama** | Magonjwa ya kawaida ya wanyama katika mikoa mbalimbali ni pamoja na Kichaa cha mbwa (mikoa yote), Kimeta (Manyara, Arusha, na Kilimanjaro), Homa ya Bonde la Ufa (Dodoma, Arusha, Manyara), Ugonjwa wa Miguu na Midomo (Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Mara, Shinyanga na Tabora). Ugonjwa wa Kimeta uliripotiwa wilayani Kiteto mwezi Aprili 2018 ambapo watu 8 walikufa na kaya 62 kuathirika kutokana na kula nyama iliyoambukizwa. Mlipuko kama huo pia ulitokea katika wilaya ya Moshi mnamo Februari 2019, Wilaya ya Rombo mnamo 2021 ambapo watu 2 walikufa kutoka kila wilaya. |
| **Visumbufu vya mazao** | Makadirio ya athari za milipuko ya visumbufu vya mazao ni wastani kwa upotevu wa mazao kati ya asilimia 30 - 40. Uvamizi wa viwavijeshi wa Marekani mwaka 2017, uliathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mazao katika mikoa ya Geita, Rukwa, Kagera, Pwani, Simiyu, Mwanza, Morogoro, Kilimanjaro, na Njombe, na unachangiwa na ukosefu wa ulinzi wa kutosha dhidi ya wadudu waharibifu na magonjwa, pamoja na hali duni, taratibu na teknolojia za utunzaji wa mazao baada ya kuvuna. Wadudu waharibifu wa kawaida ni pamoja na nzige (Katavi, Rukwa, Kigoma, Tabora na Dodoma), viwavi jeshi (mikoa yote), Quelea quelea (Dodoma, Singida, Mbeya, Kilimanjaro) na mnyauko wa ndizi, virusi vya “mosaic” cha muhogo (Kagera na Mara). |
| **Milipuko ya magonjwa ya binadamu** | Kipindupindu, Homa ya Mapafu na magonjwa mengine yanayoibuka kama vile homa ya Dengue, UVIKO -19 na Chikungunya yana hatari kubwa kwa maisha ya binadamu na uchumi, na kusababisha magonjwa na vifo vingi. Hadi sasa, mlipuko wa muda mrefu zaidi wa kipindupindu kuripotiwa nchini ni ule ulioanza Agosti 2015 na kumalizika Desemba 2018 na kusababisha vifo vya watu 550 na kuathiri watu 33,319 katika wilaya 129. |
| **Kimbunga cha tropiki** | Vimbunga vya kitropiki vina uwezekano mkubwa wa kutokea na kusababisha uharibifu mkubwa kwa maisha ya watu na miundombinu kiasi kwamba karibu kila mwaka, maeneo tofauti ya pwani ya nchi, haswa maeneo ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam huathirika zaidi. |

| Hatari | Maelezo |
| --- | --- |
| **Upepo mkali** | Maeneo yanayokabiliwa na upepo mkali zaidi nchini ni katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Songwe. Matukio ya upepo mkali yalirekodiwa katika wilaya za Nkasi, Ukerewe, Rorya na Momba na Manispaa ya Ilemela na Sumbawanga mwaka 2019 na 2020 na kuharibu nyumba 866 na kusababisha vifo vya watu 3 na kujeruhi ya watu 20. |
| **Mafuriko** | Mafuriko ni hali halisi ya kila mwaka kwa maeneo mengi nchini Tanzania na yameigharimu nchi zaidi katika hasara ya maisha, uharibifu wa miundombinu na kuzorota kwa uchumi. Mafuriko ya ghafla ni ya kawaida sana katika maeneo ya mabondeni hasa mijini. Mikoa inayokumbwa na mafuriko zaidi nchini ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Mtwara, Arusha, Lindi na Iringa. Nchi imekumbwa na mafuriko katika wilaya tofauti kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, ambayo yalisababisha vifo vya watu 307, watu 317,907 na kuharibu nyumba 50,588. |
| **Ukame** | Mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira yanasababisha uwezekano mkubwa wa kutokea kwa ukame na madhara makubwa katika usalama wa chakula na maji hasa katika maeneo ya mikoa ya kaskazini na kati ikiwemo Arusha, Manyara, Shinyanga, Simiyu na Dodoma. Matukio ya ukame yaliyotokea wilayani Bahi mkoani Dodoma mwaka 2005/2006 yalisababisha vifo vya ng'ombe 4871 na mbuzi na kondoo 1974. Ukame mwingine mkubwa katika mikoa ya Arusha na Manyara mwaka 2008/2009 ulisababisha vifo vya ng’ombe 56,585, mbuzi 39,766 na kondoo 28,883 wilayani Monduli na ng’ombe 231,832, mbuzi 171,435 na kondoo 92,235 wilayani Longido. Katika mwaka 2021/2022 matukio ya ukame yalisababisha vifo vya mifugo 308,720 wakiwemo ng’ombe, mbuzi, kondoo na punda katika mkoa wa Kilimanjaro (Same, Siha na mwanga), Pwani (Bagamoyo, Kibaha, Kibiti, Kisarawe, Rufiji na Chalinze) na Tanga (Kilindi, na Handeni, |
| **Tetemeko la ardhi** | Maeneo nchini ambayo yamo ndani ya Mfumo wa Ufa wa Afrika Mashariki huwa yanapatwa na tetemeko la ardhi. Matetemeko ya ardhi yaliripotiwa Kaskazini mwa Dodoma Julai 2002 (ukubwa 5.6), Ziwa Tanganyika mwezi Desemba 2005 (ukubwa wa 6.8), Ziwa Natron Julai 2007 (ukubwa wa 5.9), |

| Hatari | Maelezo |
|---|---|
| | mkoani Mwanza Mei 2017 (ukubwa 5.0), Sumbawanga9 Machi 20 5.5) na mkoa wa Kagera Septemba 2016 (ukubwa 5.9). Tetemeko la ardhi lililotokea mkoani Kagera mwaka 2016 likiua watu 17, kujeruhi 440 na kuathiri watu 117,721, kuharibu nyumba 2,072 na majengo ya umma 2,191. Tukio lingine la tetemeko la ardhi lililotokea mwaka 2017 huko Mwanza liliua mtu mmoja na kujeruhi watu 2 na kuharibu baadhi ya majengo katika shule 4. Tukio la tetemeko la ardhi huko Bariadi Mei 2002 liliua watu 2 na kujeruhi watu 5, kuharibu 690 na kuharibu nyumba 636. |
| **Maporomoko ya udongo** | Wakati matukio ya maporomoko ya ardhi ni ya nadra nchini Tanzania, bado kuna uwezekano wa kutokea maporomoko ya ardhi katika baadhi ya maeneo kutokana na shughuli za kiuchumi kama vile kilimo cha mifereji katika maeneo ya miinuko, ukataji miti, ujenzi, uchimbaji madini, kwa kutaja machache tu. Mwaka 2009, maporomoko ya udongo katika eneo la Kilimanjaro yalisababisha vifo vya watu 24 na kuua ng'ombe 60, huku pia yakiharibu kilomita 15 za barabara na mabwawa 15 ya umwagiliaji kutokana na athari iliyoambatana na mtiririko wa tope. Matukio ya maporomoko ya ardhi yaliripotiwa pia huko Makete mwaka 2010; Manispaa ya Arusha Aprili 2019 ambapo watu 3 walikufa na 2 kujeruhiwa; Wilaya ya Mbogwe Oktoba 2019 ambapo watu 2 walikufa; Ludewa mnamo Machi 2020 ambapo watu 2 walikufa na 5 kujeruhiwa, na nyumba 13 ziliharibiwa. |
| **Moto wa nyika na mijini** | Moto mijini ni mojawapo ya hatari za kawaida na kwa kawaida husababishwa na masuala ya matumizi ya umeme na mafuta kutokana na ukuaji wa haraka wa miji na ongezeko la watu. Matukio ya moto huripotiwa kutoka karibu mikoa yote nchini Tanzania lakini hutokea mara nyingi katika mikoa yenye watu wengi kama vile Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Msururu wa matukio ya moto shuleni kuanzia 2016 hadi 2020 yamesababisha uharibifu katika wa shule 34 za msingi na sekondari. Mlipuko wa moto katika Manispaa ya Arusha Machi 2020 uliharibu soko la Samunge lenye eneo la ekari 3.8. Mlipuko wa lori la mafuta katika Manispaa ya Morogoro mwaka 2019 uliua watu 105. |

| Hatari | Maelezo |
|---|---|
| | Moto wa nyika unaweza kusababishwa na mambo ya asili kama vile umeme na milipuko ya volkeno na mambo yanayosababishwa na binadamu kama vile uvutaji sigara na uchomaji moto, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa binadamu na mazingira na matukio ya kawaida katika mikoa ifuatayo: Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Morogoro, Lindi, Njombe, Songea, Katavi, Rukwa, Kigoma na Tabora. |
| **Dharura za nyuklia na radiolojia** | Kuzuka kwa dharura za radiolojia na nyuklia kunaweza kuwa kama matokeo ya majanga ya asili (yaani matetemeko ya ardhi, mafuriko, n.k) na au hatari za kawaida ikiwa ni pamoja na moto katika vituo vyenye vyanzo vya mionzi. Nyingine ni pamoja na matumizi mabaya ya vyanzo vya mionzi wakati wa maombi ya kawaida ya viwandani au ya matibabu, ajali wakati wa usafiri na katika maeneo yenye migogoro ya kijeshi au vitendo viovu vinavyohusisha vyanzo vya mionzi. Kutokana na ongezeko kubwa la matumizi ya vifaa vya mionzi kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta mbalimbali zikiwemo madini, viwanda, afya na kilimo, uwezekano wa kuathiriwa na mionzi yenye kiwango kikubwa na kusababisha madhara makubwa kwa wakazi na wale wanaofanya kazi katika sekta hizo ni mkubwa na baadaye inaweza kusababisha madhara makubwa kiafya, uharibifu wa mazingira, majeraha na hata vifo vya watu. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 1996-2020 jumla ya kesi 16 za usafirishaji haramu wa vifaa vya mionzi zilikamatwa zikiwa zinapitia Tanzania; shehena hizo haramu mara nyingi huhusishwa na nia ya kusababisha vitendo vya uhalifu (asilimia 81 ya kesi hizi zilikamatiwa katika jiji la Dar es Salaam). |
| **Kumwagika kwa mafuta na kuvuja kwa gesi** | Kumwagika kwa mafuta kunaweza kusababishwa na ushushaji wa mafuta yasiyosafishwa kutoka melini, matanki ya mafuta yaliyopo pwani, mitambo ya kuchimba visima, na vile vile kumwagika kwa bidhaa za petroli iliyosafishwa (kama vile petroli, dizeli, na gesi) na bidhaa zao za ziada, mafuta mazito zaidi yanayotumiwa na meli kubwa kama vile mafuta ya "bunker", au kumwagika kwa takataka yoyote ya mafuta au mafuta taka. Mafuta yaliyomwagika hupenya ndani ya manyoya ya ndege na ngozi ya mamalia, kupunguza uwezo wake wa |

| Hatari | Maelezo |
|---|---|
| | kujihami na joto, na kuwafanya wawe katika hatari zaidi ya kushuka kwa joto na kupungua kwa kasi kwa maji. Uchimbaji wa haidrokaboni pamoja na viwanda vyake vilivyounganishwa chini ya mkondo wa bahari hubeba hatari za kimazingira na hatari nyinginezo. Hivi sasa, shughuli nyingi za utafiti wa haidrokaboni nchini zinafanyika nje ya bahari katika Bahari ya Hindi na huko ndiko ugunduzi mkubwa wa gesi asilia umepatikana. |
| **Matukio ya ajali** | Ajali ni tukio lisilotarajiwa na lisilopangwa ambalo hutokea kutokana na shughuli mbalimbali na kusababisha madhara ya kimwili (jeraha au kifo) kwa mtu binafsi, uharibifu na upotevu wa mali, hasara, au mchanganyiko wa madhara haya.<br><br>Magari yanatumika kusafirisha vifaa vizito kwa shughuli za uchimbaji madini na viwandani pamoja na mizigo mizito ya taka na vifaa hatarishi. Ajali za magari pamoja na na kuhatarisha Maisha ya watu, zinaweza kusababisha athari za mazingira kutokana na kumwagika kwa mizigo na/au mafuta.<br><br>Kutokana na nyakati za mawimbi makubwa ya Bahari, Maziwa na Mito, makosa ya kibinadamu au mambo yaliyo nje ya uwezo wa mwanadamu, maji haya yamekuwa chanzo kikubwa cha kupoteza maisha ya watu na mali zao. Licha ya maendeleo makubwa katika teknolojia ya usafiri wa baharini na hatua za usalama zilizoboreshwa, Bahari, Maziwa na Mito inaweza kuwa maeneo hatari sana kwa ajali za vivuko (feri) na kusababisha maafa ya kusikitisha. Mifano ya hivi karibuni ya ajali za baharini ni pamoja na MV Spice Islander iliyozama Septemba 2011, kuzama kwa MV Skagit Julai 2012, MV. Bukoba mwaka 1995 na Kivuko cha MV. Nyerere mwaka 2018. |
| **Ugaidi** | Ugaidi ni uhalifu ulioratibiwa na uchokozi wa kikatili dhidi ya taasisi za serikali na jamii. Tanzania iko katikati mwa Ukanda wa Maziwa Makuu ambayo imekuwa kitovu cha vita vya silaha na mashambulizi makubwa ya kigaidi. Mashambulizi ya wakati huo dhidi ya Balozi za Marekani jijini Dar-es-Salaam mwaka 1998 ni kielelezo cha uwezekano wa Tanzania kukabiliwa na mashambulizi ya kigaidi. Ugaidi unaweza kuhusisha vitendo vya |

| Hatari | Maelezo |
|---|---|
| | uharibifu kwa kutumia silaha za maangamizi makubwa ikiwa ni pamoja na mawakala wa kemikali, hatari za kibiolojia, ajenti za radiolojia, vifaa vya nyuklia au vilipuzi. Kusudi kuu la gaidi ni kueneza hofu katika eneo lililodhamiriwa. |

**C. Uchambuzi wa hatari za maafa**

Mnamo 2020 majanga yaliyoainishwa katika Jedwali Na. 1 yalifanyiwa tathmini kwa njia ya utambuzi wa hatari na wataalam kutoka katika taasisi mbalimbali kwa kutumia bangokitita la uchambuzi wa hatari. Kila janga lilifanyiwa tathmini kulingana na: (i) uwezekano wa kutokea, (ii) matokeo kulingana na uzito wa athari kwa maisha, afya, miundombinu, uchumi na jamii na uwiano wa kiwango cha hatari kulingana na hatua hizo mbili. Jedwali Na. 2 linatoa matokeo ya tathmini hii.

**Jedwali Na. 2: Bangokitita la Tathmini ya Uchambuzi wa Hatari nchini**

| HATARI | UWEZEKANO | MATOKEO | KIWANGO CHA HATARI |
|---|---|---|---|
| **Magonjwa ya milipuko ya wanyama** | Kiasi | Makubwa | Juu sana |
| **Milipuko ya wadudu** | Yawezekana | Makubwa | Juu sana |
| **Ugonjwa wa magonjwa ya binadamu** | Yawezekana | Makubwa | Juu sana |
| **Vimbunga vya kitropiki** | Yawezekana | Makubwa | Juu sana |
| **Upepo mkali** | Kiasi | Wastani | Juu sana |
| **Mafuriko** | Yawezekana | Makubwa | Juu sana |
| **Ukame** | Inawezekana | Makubwa | Juu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Matetemeko ya ardhi** | Kiasi | Ya juu | Juu sana |
| **Maporomoko ya ardhi** | Kiasi | Makubwa | Juu sana |
| **Moto wa nyika na mijini** | Kiasi | Makubwa | Juu sana |
| **Nyuklia na radiolojia** | Kiasi | Makubwa | Juu sana |

## 5. MIPANGO TARAJIWA

A. Tanzania Bara itaendelea kuwa katika hatari ya majanga yaliyoelezwa katika jedwali Na.2 na pia mengine yanaweza kuongezeka baadaye kutokana na kubadilika kwa hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi.

B. Maafa yanaweza kutokea wakati wowote na mahali popote nchini. Mara nyingi, utoaji wa taarifa za tahadhali za awali kwa umma na utekelezaji wa hatua za kujiandaa zinawezekana kufanyika. Hata hivyo, baadhi ya maafa hutokea bila pasipo kuwepo kwa tahadhari ya kutosha au bila tahadhari kabisa.

C. Kwa kuwa inachukua muda mrefu kupata usaidizi kutoka nje, ni muhimu kuwa tayari kuchukua hatua za awali za kukabiliana na maafa kwa njia ya kujitegemea.

D. Maafa yanaweza kusababisha vifo na majeraha mengi, uharibifu wa mali, uharibifu wa mazingira na usumbufu katika mifumo ya kawaida ya kijamii.

E. Kiwango cha majeruhi na uharibifu kitahusishwa na sababu kama vile wakati wa kutokea janga, ukubwa wa athari, hali ya hewa, msongamano wa watu, miundombinu iliyo katika hali hatarishi, na uwezekano wa kutokea kwa matukio mengine kama vile matukio ya moto na mafuriko. Aidha, kiwango cha uharibifu na visababishi kitategemeana na hatari zilizopo na uwezekano wa kuathirika au kudhurika.

F. Idadi kubwa ya majeruhi, uharibifu mkubwa wa majengo na miundombinu muhimu, na uharibifu wa huduma muhimu za umma utazidi uwezo wa serikali kukidhi mahitaji kwa mazingira yanayohusika, Rais atatangaza hali ya hatari.
G. Taasisi za serikali na wadau mbalimbali zitahitaji kukabiliana na maafa kwa muda mfupi na kwa wakati unaofaa.
H. Hatua thabiti za kuzuaia au kupunguza madhara zinaweza kuzuia au kupunguza hasara zinazohusiana na maafa. Hata hivyo, upangaji wa kina wa usimamizi wa maafa, mafunzo kwa watoa huduma za dharura na wafanyakazi wengine, kufanya mazoezi ya dharura ya mara kwa mara na kujenga ufahamu wa umma kunaweza kuboresha utayari wa kukabiliana na maafa katika jamii husika.
I. Wadau wote katika ngazi zote wanapaswa kufahamu uwezekano wa kutokea kwa maafa na pia wanapaswa kufahamu wajibu wao katika utekelezaji wa mpango huu na kutimiza majukumu haya ipasavyo pale inapohitajika.
J. Kuzingatia uwezo na upatikanaji wa rasilimali, ikiwa utatumika ipasavyo, itapunguza upotevu wa maisha na uharibifu wa mali katika tukio la maafa makubwa. Hii lazima ijumuishe ushirikiano na watendaji wa sekta binafsi na mashirika yasiyo ya serikali na wadau wa maendeleo.

## 6. DHANA YA KUKABILI

A. Ni jukumu la Serikali kuandaa mpango wa kina wa usimamizi wa maafa ambao unakidhi mahitaji ya dharura ya wale ambao wameathiriwa au wanaweza kuathiriwa na maafa. Maafa yanapozidi uwezo wa Serikali wa kukabiliana nayo, usaidizi utaombwa kutoka kwa nchi nyingine na Mashirika yanayofaa ya Kikanda na Kimataifa ya kutoa huduma za kibinadamu.
B. Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa ina jukumu la kuratibu masuala yote ya usimamizi wa maafa nchini; ikijumuisha hatua za kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Majukumu mengine ni kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na.6 ya mwaka 2022.

C. Mpango huu umelenga katika dhana kwamba majukumu yaliyoainishwa katika mpango huu yatatekelezwa na Wizara, idara, taasisi za umma na mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo sambamba na majukumu yao ya kila siku kwa ukaribu kadri inavyowezekana. Wafanyakazi na rasilimali zilizopo katika taasisi husika zitatumika wakati wa shughuli za kujiandaa na kukabiliana na maafa.

D. Shughuli za kila siku ambazo hazichangii moja kwa moja kwa shughuli za maafa zinaweza kusimamishwa wakati wa maafa. Juhudi ambazo kwa kawaida zingehitajika kwa shughuli hizo zitaelekezwa kwenye ukamilishaji wa shughuli za maafa na idara au mtaalam anayehusika.

E. Mpango huu utatekelezwa kulingana na aina za maafa na taratibu za udhibiti zilizoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Maafa, Na.6 ya mwaka 2022.

F. Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa kupitia Kituo cha Mawasiliano na Operesheni za Dharura itapokea taarifa ya tahadhari za awali ya maafa kutoka katika chanzo chochote na kuzingatia njia sahihi ya kuthibitisha taarifa hiyo. Pale ambapo idara itakapojiridhisha kwamba hali ya dharura iliyojitokeza inaongezeka na kuwa maafa Kamati za Usimamizi wa Maafa zitaitishwa. Kamati Elekezi itamshauri Waziri Mkuu juu ya hatua za kuchukua na kwa upande wake atamshauri Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapendekezo ya Kamati Elekezi ya Taifa.

G. Baada ya kupokea taarifa hiyo na ushauri, Rais anaweza kumwelekeza Waziri Mkuu kama ataona ni muhimu Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa na Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wakati wa Maafa uanze kutumika.

H. Rais anaweza kutangaza eneo lililotokea tukio la dhaura kuwa eneo la maafa na umma hautaruhusiwa kutumia eneo hilo mapaka maelekezo yatakapotolewa vinginevyo.

## 7. MUUNDO NA MGAWANYO WA MAJUKUMU

### A. Muundo

Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa umeainisha maeneo kumi na tano (15) ya utendaji ambayo yamewekwa katika Kongani. Kongani za majukumu zinaelezea dhana ya uendeshaji na majukumu ya Taasisi Ongozi na Saidizi zinazohusika katika utekelezaji wa kazi muhimu za kukabiliana na maafa. Majukumu ya usaidizi ya kukabiliana na maafa yatahusisha Kongani zifuatazo:

Kongani 1: Maelekezo na Udhibiti
Kongani 2: Mawasiliano na Tahadhari za Awali
Kongani 3: Uhamishaji
Kongani 4: Uzimaji Moto
Kongani 5: Usimamizi wa Sheria, Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali Zao
Kongani 6: Huduma za Afya na Matibabu
Kongani 7: Utafutaji na Uokoaji
Kongani 8: Makazi ya Muda na Huduma kwa Waathirika
Kongani 9: Taarifa na Tahadhari kwa Umma
Kongani 10: Tathmini ya Uharibifu na Mahitaji
Kongani 11: Ujenzi na Uhandisi
Kongani 12: Huduma za Nishati na Maji
Kongani 13: Usimamizi na Usambazaji wa Rasilimali
Kongani 14: Usafirishaji
Kongani 15: Huduma za afya ya akili na ushauri wa kisaikolojia

### B. Mgawanyo wa Majukumu

(i) Kwa kila Kongani, utekelezaji wa majukumu wenye mafanikio unahitaji juhudi zilizoratibiwa vizuri kutoka Serikalini na kwa Mashirika kadhaa yasiyo ya Serikali. Ili kuwezesha juhudi zilizoratibiwa, Maafisa waliochaguliwa na kuteuliwa, Wakuu wa Idara na Taasisi za umma, na wafanyikazi wengine wanapewa jukumu la msingi la kupanga, kutekeleza na kuratibu majukumu mahususi ya kushughulikia maafa.

(ii) Jukumu la kimsingi kwa kila Kongani wakati wa maafa litakabidhiwa kwa mtu binafsi kutoka katika Idara au Taasisi ambayo ana jukumu la kisheria la kutekeleza kazi hiyo au ana ujuzi unaofaa zaidi. Idara,

taasisi na wadau wengine wanaweza kupewa majukumu ya usaidizi kwa shughuli maalum za menejimenti ya maafa. Jedwali Na. 3 linatoa muhtasari wa majukumu ya menejimenti ya maafa kwa idara na taasisi muhimu za Serikali na mashirika mengine.

(iii) Itakuwa ni jukumu la idara hizo, taasisi au mashirika mengine yenye jukumu la msingi au la usaidizi kudumisha matumizi ya miongozo ya sasa ya uendeshaji na orodha za ukaguzi ambazo zinaeleza jinsi kazi waliyokabidhiwa itatekelezwa katika mpango huu.

(iv) Idara na watu binafsi waliopewa majukumu ya menejimenti ya maafa watashughulikia mahitaji ya makundi yenye mahitaji maalum.

## 8. MAJUKUMU YA KONGANI

**Jedwali Na. 3: Taratibu za Kiutendaji kwa kila Kongani- Wadau, Maelezo na Kazi**

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| ***Kongani Na.1: Maelekezo na Udhibiti*** <br> ***Maelezo:*** *Kongani hii inasaidia juhudi za kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa kuratibu upatikanaji wa rasilimali na shughuli zitakazotekelezwa na wadau mbalimbali.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Menejimenti ya Maafa <br><br> **Naibu Taasisi Ongozi:** Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya | **Taasisi Saidizi:** Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kamati za Usimamizi wa Maafa za Kata na Vijiji na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:** <br> 1) Kuweka lengo na vipaumbele vya programu za kujiandaa na kukabiliana na maafaa na kuweka mwongozo wa jumla wa kisera wa namna ya kutekeleza programu hizo. <br> 2) Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kukabiliana na maafa. <br> 3) Kutoa taarifa kwa umma wakati wa hali ya dharura. <br> 4) Kuelekeza uamshwaji wa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura. <br> 5) Kuainisha mahitaji ya watumishi, zana na vifaa. <br> 6) Kupanga kazi kwa idara, wakala na taasisi za kujitolea. <br> 7) Kuratibu mipango na shughuli za |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | kujiandaa na kufanya maboresho ya mpango huu.<br>8) Kupanga mafunzo kwa wataalamu wa kukabili maafa.<br>9) Kuratibu makundi ya kujitolea ya ndani na ya kimataifa na makundi yanayotoa misaada ya kibinadamu wakati wa Operesheni za maafa. |
| ***Kongani #2: Mawasiliano na Tahadhari***<br>***Maelezo:*** *Kongani ya Mawasiliano na Tahadhari inawatahadharisha wataalamu waliopo katika serikali za mitaa kuhusu hali ya maafa, inasambaza taarifa za onyo na maagizo kutoka Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura, kongani zinazohusika na jamii kupitia mifumo ya utoaji wa tahadhari iliyopo, kubainisha mifumo ya mawasiliano inayopatikana nchini katika ngazi zote.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Menejimenti Maafa<br><br>**Naibu Taasisi Ongozi:** Wizara yenye dhamana ya Habari na Mawasiliano na Taasisi zinazohusika na Tahadhari za Awali. | **Taasisi Saidizi**: Idara ya Huduma za Habari, Idara ya Mawasiliano, Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Wizara yenye dhamana ya Afya, Wizara inayohusika na Mifugo, Wizara inayohusika na Kilimo, Wizara inayohusika na Maji, Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa | **Kazi:**<br>1) Kupokea taarifa za tahadhari na matukio ya maafa.<br>2) Kuwataarifu maofisa muhimu katika ngazi ya chini kuhusu tukio la maafa.<br>3) Kusambaza taarifa za tahadhari na maelekezo kwa umma kupitia mifumo ya tahadhari iliyopo.<br>4) Kusambaza taarifa ya tahadhari na maelekezo |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | na taasisi nyingine zinazohusika. | kwa maeneo muhimu kama shule, magereza, nyumba za malezi, vituo vya malezi ya kutwa na hospitali.<br>5) Kutambua mifumo ya mawasiliano iliyopo katika nchi katika ngazi zote na kuelewa mwingiliano wa mifumo hiyo na kuhakikisha mwingiliano katika uendeshaji wake.<br>6) Kuandaa utaratibu wa matumizi bora ya mifumo mbalimbali ya mawasiliano iliyopo nchini wakati wa maafa.<br>7) Kutambua na kutekeleza njia za kufanikisha mawasiliano wakati wa maafa ikijumuisha msaada wa taasisi za kujitolea. |
| ***Kongani #3: Uhamishaji***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inalenga kusimamia zoezi la kuhamisha wananchi kutoka kwenye maeneo hatarishi. Kazi za kongani hii zinajumuisha utambuzi wa maeneo ambayo ulifanyika au unatarajiwa kufanyika, kubainisha idadi ya watu walio hatarini, kufanya mipango ya uokoaji, kuandaa utaratibu rahisi wa mipango kwa ajili ya uhamishaji wa dharura.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Jeshi la Polisi Tanzania<br><br>**Naibu Taasisi Ongozi:** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania | **Taasisi Saidizi:** Ofisi ya Waziri Mkuu(Idara ya Menejimenti ya Maafa), Chama cha Skauti Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa), Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)*[1] na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kutambua maeneo ambayo uhamishwaji ulifanyika au unatarajiwa kufanyika na kutambua idadi ya watu iliyoko katika hatari.<br>2) Kuandaa mipango ya uhamishaji kwa maeneo yajulikanayo kuwa katika hatari ikijumuisha uchaguzi wa njia na kutambua |

[1]*TPDF itahusika tu katika tukio ambalo mamlaka za kiraia na wafanyakazi wamezidiwa.

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | mahitaji ya kudhibiti msongamano au misafara.<br>3) Kuunda utaratibu rahisi wa mipango kwa ajili ya uhamishaji wa dharura.<br>4) Kufanya mipango ya uhamishaji kwa maeneo yenye mahitaji ya huduma maalum (shule, hospitali, nyumba za malezi, na taasisi nyinginezo)<br>5) Kuratibu usafiri kwa kundi la watu wanaohama.<br>6) Kuratibu huduma za usalama kwa maeneo yaliyohamishwa na makazi ya muda. |
| ***Kongani #4: Kukabili Moto***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii ina jukumu la kusimamia shughuli za kuzuia moto, kutoa maelekezo na udhibiti wa moto, kufanya tathmini ya upelelezi na uharibifu baada ya tukio na ukaguzi wa usalama wa makazi ya muda.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania | **Taasisi Saidizi:** Jeshi la Polisi Tanzania - Huduma za Dharura, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Mamlaka za Maji, Makampuni Binafsi ya Zimamoto na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kuratibu shughuli za udhibiti wa moto na kujikinga na moto.<br>2) Kuratibu shughuli za kuzuia na kujikinga na moto.<br>3) Kukabiliana na maafa yanayosababishwa na uvujaji wa mafuta na vitu vingine hatarishi. |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 4) Kukabiliana na vitendo vya kigaidi.<br>5) Kusaidia katika zoezi la uhamishaji.<br>6) Kufanya upelelezi na tathmini ya uharibifu baada ya tukio la moto<br>7) Ukaguzi wa usalama dhidi ya majanga ya moto katika makazi ya muda.<br>8) Kuandaa na kutunza orodha ya rasilimali za uokoaji dhidi ya moto. |
| ***Kongani#5: Utekelezaji wa Sheria***<br>1) ***Maelezo:*** *Kongani hii ina jukumu la kusimamia sheria na taratibu, udhibiti wa msongamano wa magari, kukabiliana na matukio ya kigaidi, kusimamia usalama wa vifaa muhimu, maeneo yaliyohamwa na makazi ya muda, kudhibiti kufikiwa kwa maeneo kuathiriwa na usaidizi wa kufanya upelelezi na tathmini ya uharibifu baada ya matukio.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Jeshi la Polisi Tanzania | **Taasisi saidizi:** Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Magereza Tanzania na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>2) Kuratibu operesheni za utekelezaji wa sheria<br>3) Kusimamia sheria na taratibu.<br>4) Udhibiti wa msongamano wa magari.<br>5) Kukabiliana na matukio ya kigaidi.<br>6) Kutoa ulinzi kwa vifaa muhimu, maeneo yaliyohamwa na malazi ya muda |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 7) Kudhibiti kufikiwa kwa maeneo yaliyoathiriwa.<br>8) Kusaidia katika utoaji wa tahadhari ya mapema.<br>9) Kufanya upelelezi na tathmini ya uharibifu baada ya tukio na kutunza vithibitisho endapo maafa husika yatahushiswa na vitendo vya kihalifu.<br>10) Kuandaa na kutunza orodha ya rasilimali ya utekelezaji wa sheria. |
| ***Kongani #6: Huduma za Afya na Matibabu***<br>***Maelezo:*** *Kongani ya hii inaratibu huduma za afya na matibabu wakati wa hali ya maafa, utoaji wa taarifa na elimu ya afya kwa umma, ukaguzi wa chakula na maji vinavyosambazwa kwa waathirika na kuratibu utambuzi na maziko ya waathiriwa waliopoteza maisha.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Wizara yenye dhamana ya afya | **Taasisi Saidizi:** Wizara zinazohusika na Mifugo, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia wa Serikali, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayohusiana na Afya, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Kimataifa na Mashirika ya Huduma Binafsi za Dharura na | **Kazi:**<br>1) Kuratibu huduma za afya na matibabu wakati wa hali za maafa.<br>2) Kutoa taarifa na elimu ya afya kwa umma.<br>3) Ukaguzi wa chakula na maji vinavyosambazwa kwa waathirika.<br>4) Kuandaa kanuni na maagizo ya afya ya umma wakati wa maafa. |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | wadau au taasisi nyingine zinazohusika. | 5) kuratibu utambuzi na maziko ya waathiriwa waliopoteza maisha<br>6) Kukusanya, kutunza na kulinda taarifa muhimu za waathirika zinazohusu afya.<br>7) Kufanya tathmini na uchambuzi wa maombi ya huduma za afya na matibabu yaliyowasilishwa pamoja na kufanya mapitio ya tathmini ya hali ya huduma za afya. |
| ***Kongani #7: Utafutaji na Uokoaji***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inaratibu na kuendesha shughuli za utafutaji na uokoaji, inaainisha mahitaji na rasilimali maalum ili kusaidia shughuli za utafutaji na uokoaji, na kuratibu misaada ya kitaalamu na vifaa vya utafutaji na uokoaji kutoka nje.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania | **Taasisi Saidizi:** Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Jeshi la Polisi Tanzania, Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa, Chama cha Skauti Tanzania, Mashirika ya Kimataifa na ya Umoja wa Mataifa, Kampuni ya Wakala wa Meli Tanzania, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Makampuni Binafsi, Vitengo vya Usimamizi wa Ufukwe na Watu Wenye Ujuzi na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na wadau au taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kuratibu na kuendesha shughuli za utafutaji na uokoaji.<br>2) Kuainisha mahitaji ya rasilimali muhimu kusaidia shughuli za uokoaji.<br>3) Kuratibu msaada wa kitaalamu na vifaa vya utafutaji na uokoaji kutoka nje.<br>4) Kuanzisha na kusimamia timu ya utafutaji na uokoaji ikiwa pamoja na kujumuisha shughuli za kabla ya maafa kutokea kama vile mafunzo, ununuzi wa vifaa na tathmini ya utayari wa kukabiliana na maafa. |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| ***Kongani #8: Malazi na Uhifadhi wa Makundi ya Watu***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inaratibu na kuendesha shughuli za malazi na uhifadhi wa makundi ya watu, inaainisha maeneo ya uhifadhi wa watu wakati wa maafa, inaainisha vyanzo vya mahitaji ya msingi kwa waathirika wa maafa kama vile chakula, nguo na vifaa vya usafi wa mazingira na kuratibu mahitaji maalum ya huduma kwa waathirika wa maafa.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Ofisi ya Waziri Mkuu | **Taasisi Saidizi:** Wizara zenye dhamana na Ustawi wa Jamii, Maji, Nishati, Mazingira, Afya, Kilimo, Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Polisi Tanzania, Sekretarieti za Mikoa, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, Chama cha Skauti Tanzania, Sekta Binafsi/ Zisizo za serikali/Imani/Jumuiya za Kiraia/ Mashirika na watu wa kujitolea wa kijamii, Mashirika ya Kimataifa na Umoja wa Mataifa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, wadau na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kuandaa na kutekeleza mpango wa malazi na uhifadhi watu wakati wa maafa.<br>2) Kuratibu na kutekeleza shughuli za utoaji wa huduma ya makazi ya muda yanayohusisha watu wengi kwa ushirikiano na wakala za uokoaji na makundi ya kujitolea idara nyingine.<br>3) Kuainisha maeneo ya uhifadhi wa watu wakati wa maafa.<br>4) Kuainisha vyanzo vya mahitaji ya msingi kwa waathirika wa maafa kama vile chakula, nguo na vifaa vya usafi wa mazingira Kuhakikisha upatikanaji wa chakula wakati wa maafa.<br>5) Kuratibu mahitaji maalum kwa waathirika wa maafa kama watoto, waja wazito, wazee, walemavu, watu wengine wenye mahitaji maalum.<br>**6)** kuratibu mahitaji maalum ya huduma kwa waathirika wa maafa, na kuratibu huduma za kisaikolojia kwa waathiriwa wa maafa na |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| ***Kongani #9: Mawasiliano, Taarifa na tahadhari kwa Umma***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inaanzisha Kituo cha Pamoja cha Utoaji wa Taarifa, kufanya uhamasishaji pamoja na programu za uelimishaji wa umma kuhusu masuala ya majanga, kukusanya na kutoa taarifa na maagizo kwa umma wakati wa hali ya maafa na kujibu maswali yanayohusiana operesheni wakati wa maafa, kuandaa na kutoa taarifa na maelekezo kwa umma na vyombo vya habari wakati wa hali ya maafa, kufuatilia vyombo vya habari ili kubaini taarifa potofu na kutoa ufafanuzi kwa umma ili kudhibiti uvumi.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Wizara yenye dhamana ya Habari | **Taasisi Saidizi:** OWM, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sekretarieti za Mikoa nana Serikali za Mitaa, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Waendeshaji/Wamiliki wa Mitandao ya Simu, Vyombo vya Habari na Wadau au taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kuanzisha Kituo cha Pamoja cha Utoaji wa Taarifa<br>2) Kuendesha programu za uelimishaji wa umma kuhusu masuala ya majanga.<br>3) Kukusanya na kutoa taarifa na maelekezo kwa umma kuhusu wakati wa maafa na kujibu maswali yanayohusu operesheni wakati wa maafa.<br>4) Kuandaa na kutoa taarifa na maelekezo kwa umma na vyombo vya habari wakati wa hali ya maafa.<br>5) Kuandaa mikutano ya ufafanuzi kwa vyombo vya habari.<br>6) Kufuatilia taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari ili kufahamu habari za upotoshaji kuhusu tukio.<br>7) Kujibu maswali yanayohusiana na kukabili maafa.<br>8) Kusimamia kituo kinachopokea simu kwenye namba ya dharura.<br>9) Kuhakikisha umma unapata taarifa za mara |

<table>
<tr><th>TAASISI ONGOZI</th><th>TAASISI SAIDIZI</th><th>KAZI</th></tr>
<tr><td></td><td></td><td>kwa mara kuhusu hali ya maafa na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nayo, ili kuepusha kuenea kwa uvumi na kusababisha taharuki kwa umma.<br>10) Kuhakikisha kuwa mifumo ya kutuma na kupokea taarifa inafanya kazi.<br>11) Kukusanya na kuandaa taarifa za hali ya maafa.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Kongani #10: Tathmini ya Uharibifu na Mahitaji<br>Maelezo: Kongani hii inahusu utengenezaji wa hadidu za rejea za kufanya tathmini ya uharibifu na mahitaji, kuanzisha na kujenga uwezo wa Timu za Tathmini ya uharibifu na mahitaji. Kutathmini na kuunganisha taarifa ya uharibifu wa mali za umma na za watu binafsi, mazingira na mahitaji ya waathirika wa maafa na kuandaa na kutekeleza programu zitakazojibu mahitaji hayo.</td></tr>
<tr><td>Taasisi Ongozi: Ofisi ya Waziri Mkuu</td><td>Taasisi Saidizi: Taasisi Ongozi na Taasisi Saidizi wa kongani zote na taasisi nyingine zinazohusika.</td><td>Kazi:<br>1) Kuandaa hadidu za rejea za kuendesha tathmini ya uharibifu na mahitaji.<br>2) Kuanzisha na kuelimisha timu ya tathmini ya uharibifu na mahitaji.<br>3) Kuratibu juhudi za timu ya kutathmini ya uharibifu na mahitaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.<br>4) Kutathmini na kuunganisha taarifa ya uharibifu wa mali za umma na za watu binafsi na mazingira na mahitaji ya waathirika wa maafa na kuandaa na kutekeleza programu zitakazojibu mahitaji hayo.<br>5) Kukusanya taarifa ambazo zitatumika kwa ajili ya kuomba misaada ndani na nje ya nchi ikiwa athari za maafa zipo nje ya uwezo wa nchi.</td></tr>
</table>

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 6) kukusanya na kuhifadhi takwimu zote za uharibifu unaohusiana na maafa. |
| ***Kongani #11: Shughuli za Ujenzi na Uhandisi***<br>***Maelezo**: Kongani inahusika na kulinda* rasilimali za Serikali na vifaa muhimu inapowezekana*, kutathmini uharibifu wa mitaa, madaraja, reli, vifaa vya kudhibiti mwendo na mali nyingine za umma, inaelekeza ukarabati wa muda wa vifaa muhimu, kurejesha barabara na madaraja yaliyoharibiwa, kurejesha mifumo ya majitaka, kupanga* uondoaji wa mabaki, *kutoa usaidizi wa tathmini ya jumla ya uharibifu, kutoa usaidizi wa ukaguzi wa majengo, kutoa vifaa maalum vya kusaidia shughuli za maafa kama vile udhibiti wa trafiki na shughuli za utafutaji na uokoaji.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Wizara yenye dhamana ya Ujenzi | **Taasisi Saidizi:** Wakala wa Barabara nchini, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania., Shirika la Reli Tanzania, Mamlaka ya Anga Tanzania, Wakala wa Majengo Tanzania, Shirika la Nyumba Tanzania, Bodi ya Mfuko wa Barabara, Makampuni Binafsi ya Ujenzi na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kulinda rasilimali za Serikali na vifaa muhimu inapowezekana.<br>2) Kutathmini uharibifu katika mitaa, madaraja, vifaa vya kudhibiti mwendo na mali nyingine za umma.<br>3) Kuelekeza ukarabati wa muda wa vifaa muhimu kama mabomba ya gesi, nguvu za nishati, maji, mifereji ya maji taka, mawasiliano na usafirishaji. Vifaa vingine muhimu ni pamoja na miundombinu ya Serikali kama ofisi, hospitali, vituo vya polisi na zimamoto, taasisi za elimu ya juu na shule (kwa uhifadhi wa watu wengi).<br>4) Kurejesha barabara na madaraja yaliyoharibiwa.<br>5) Kurejesha mifumo ya majitaka.<br>6) Kuandaa uondoaji wa mabaki. |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 7) Kutoa msaada kufanya tathmini ya kina ya uharibifu.<br>8) Kutoa msaada wa ukaguzi wa majengo.<br>9) Kutoa vifaa maalum kusaidia uendeshaji wa shughuli za maafa.<br>10) Kusaidia kudhibiti msongamano, utafutaji na shughuli za uokoaji. |
| ***Kongani #12: Nishati na Huduma nyinginezo***<br>***Maelezo***: *Kongani hii inahusu kuainisha vipaumbele vya kurejesha huduma za nishati na maji kwenye maeneo muhimu kama vile hospitali, kuweka utaratibu wa upatikanaji wa vyanzo vya nishati vya dharura, kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama na vyoo vya kuhamishika kwa ajili ya makazi ya muda, kufanya tathmini ya uharibifu kwenye miundombinu ya kutolea huduma za nishati na maji pamoja na kuainisha mahitaji, kukarabati na kurejesha huduma za umma, na kuratibu ushiriki wa wadau na jamii katika utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma ya nishati na maji.* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Wizara yenye dhamana ya nishati | **Taasisi Saidizi:** Shirika la Umeme Tanzania, Wakala wa Nishati Vijijini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka za Maji, Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Jeshi la Wananchi Tanzania, Makampuni Binafsi na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kuainisha vipaumbele vya kurejesha huduma za nishati na maji kwenye maeneo muhimu kama vile hospitali<br>2) Kuweka utaratibu wa upatikanaji wa vyanzo vya nishati vya dharura;<br>3) Kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama na vyoo vya kuhamishika kwa ajili ya Makazi ya Muda;<br>4) Kufanya tathmini ya uharibifu kwenye miundombinu ya kutolea huduma za nishati na maji pamoja na kuainisha mahitaji; |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 5) Kuratibu ushiriki wa wadau na jamii katika utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma ya nishati na maji. |
| ***Kongani #13: Usimamizi na Usambazaji wa Rasilimali***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inahusu hesabu ya rasilimali za maafa, kuelekeza na kusambaza huduma muhimu kama vile chakula, dawa, vifaa, na wafanyakazi wa operesheni za maafa ili kukidhi mahitaji wakati wa operesheni za maafa, kuandaa na kutunza orodha ya wazabuni/wasambazaji wa vifaa vya maafa na misaada, kuratibu shughuli za ununuzi wa dharura, kuratibu usafirishaji, uchambuzi, uhifadhi wa muda na usambazaji wa rasilimali katika matukio ya maafa, kuandaa maeneo yatakayotumika kupokelea rasilimali pale itakapohitajika, kubainisha na kuwasilisha mahitaji na kudumisha rekodi za matumizi yanayohusiana na maafa kwa ununuzi na wafanyikazi. .* | | |
| **Taasisi Ongozi:** Ofisi ya Waziri Mkuu | **Taasisi Saidizi:** Wadau wote wa Taasisi Saidizi wametambuliwa katika kongani zote. | **Kazi:**<br>1) Kutunza orodha ya rasilimali za maafa.<br>2) kuelekeza na kusambaza huduma muhimu kama vile chakula, dawa, vifaa, na wafanyakazi wa operesheni za maafa ili kukidhi mahitaji wakati wa operesheni za maafa<br>3) Kuandaa na kutunza orodha ya wazabuni/wasambazaji wa vifaa vya maafa na misaada.<br>4) Kuratibu shughuli za ununuzi wakati wa maafa.<br>5) Kuandaa na kutunza orodha ya nguvukazi ya akiba na kuratibu majukumu ya nguvukazi ya akiba kwa idara na wakala zinazohitaji kuongezewa nguvukazi.<br>6) Kuratibu usafirishaji, uchambuzi, uhifadhi wa muda na usambazaji wa rasilimali katika matukio ya maafa. |

| TAASISI ONGOZI | TAASISI SAIDIZI | KAZI |
|---|---|---|
| | | 7) Kuandaa maeneo yatakayotumika kupokelea rasilimali pale itakapohitajika.<br>8) Kutunza orodha ya vifaa na huduma zinazotolewa, rasilimali zilizotumika na rasilimali zisizotumika.<br>9) Kutunza kumbukumbu za makisio au dhamani ya misaada iliyotolewa. |
| ***Kongani #14: Usafirishaji***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inahusu kuainisha rasilimali za usafirishaji za umma na binafsi na kuratibu matumizi yake wakati wa maafa, hasa katika kusaidia huduma za msaada wa uhamishaji kwa kaya zisizokuwa na nyenzo za usafiri. Kongani hii inaratibu matumizi ya nyenzo za usafiri kusaidia shughuli za uendeshaji wakati wa maafa na kuweka na kuhifadhi akiba ya madereva, watumishi wa ukarabati, vipuli na vifaa, na kutunza kumbukumbu za matumizi ya nyenzo za usafirishaji na watumishi.* | | |
| **Taasisi Ongozi**: Wizara yenye dhamana na Uchukuzi | **Taasisi Saidizi:** Wakala wa Ndege za Serikali, Shirika la Wakala wa Meli Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu, Shirika la Reli Tanzania, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania, Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania, Kampuni Binafsi za Usafirishaji na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kutambua rasilimali za usafirishaji za umma za ndani na nje na kuratibu matumizi yake wakati wa maafa, hasa katika kusaidia huduma za msaada wa uhamishaji kwa kaya zisizokuwa na nyenzo za usafiri.<br>2) Kuratibu matumizi ya nyenzo za usafiri kusaidia shughuli za uendeshaji wakati wa maafa.<br>3) Kuweka na kuhifadhi akiba ya madereva, watumishi wa ukarabati, vipuli na vifaa.<br>4) Kutunza kumbukumbu za matumizi ya nyenzo za usafirishaji na watumishi. |

| ***Kongani #15: Huduma ya afya ya akili na ushauri wa kisaikolojia***<br>***Maelezo:*** *Kongani hii inahusu kubuni na kutekeleza mipango na programu maalum za kuzuia na kukabiliana na athari mbaya za kisaikolojia kwa waathirika, kuhakikisha kuna utoaji wa huduma wa Afya ya Akili yenye viwango na ubora, kuanzisha Timu za Utoaji wa Huduma za Kisaikolojia katika maeneo yaliyopata maafa na utoaji wa huduma za kisaikolojia kwa watu walio katika mazingira magumu kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao.* | | |
|---|---|---|
| **Taasisi Ongozi**: Wizara yenye dhamana na Ustawi wa Jamii | **Taasisi Saidizi:**<br>Wizara zenye dhamana ya TAMISEMI, Afya, Elimu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mambo ya Ndani ya Nchi, Katiba na Sheria, Mambo ya Nje, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Fedha na Mipango na taasisi nyingine zinazohusika. | **Kazi:**<br>1) Kubuni na kutekeleza mipango na programu maalum za kuzuia na kukabiliana na athari mbaya za kisaikolojia kwa waathirika.<br>2) Kuhakikisha kuna utoaji wa huduma wa Afya ya Akili yenye viwango na ubora.<br>3) Kuanzisha Timu za Utoaji wa Huduma za Kisaikolojia katika maeneo yaliyopata maafa<br>4) Utoaji wa huduma za kisaikolojia kwa watu walio katika mazingira magumu kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao. |

## 9. MAANDALIZI NA MAPITIO YA MPANGO

A. Ofisi ya Waziri Mkuu- Idara ya Menejimenti ya Maafa itafanya mapitio ya mara kwa mara ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa kwa kushirikisha idara zote, taasisi na mashirika yasiyokuwa ya Serikali pamoja na mashirika ya kimataifa yaliyopewa jukumu la utekelezaji wa mpango huo.

B. Mpango huo utafanyiwa majaribio kila mwaka kupitia zoezi la nadharia na vitendo linalohusisha Serikali, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wadau wengine. Zoezi la nadharia na vitendo litatoa mapitio ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa kwa kuzingatia majanga mapya yanayojitokeza, uzoefu uliopatikana na mafunzo kutokana na shughuli za kukabili maafa zilizopita, mabadiliko ya sheria, mapitio ya sera na mabadiliko ya muundo wa serikali.

C. Mpango huu utapitiwa upya kila baada ya miaka mitatu.

# SEHEMU YA PILI: VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: SAA 72 ZA KWANZA ZA MAAFA

A. Saa 72 za kwanza za dharura au maafa ni kipindi muhimu zaidi katika kukabiliana na maafa. Inatambulika pia kwamba jamii ina uwezekano mkubwa wa kuwa peke yao wakati wa hatua ya awali ya maafa kadri jitihada za serikali za kukabiliana na maafa hayo zikiendelea.

B. Wakati na mara baada ya maafa makubwa kutokea, rasilimali zote huzuiliwa. Barabara zinaweza kuzuiwa, mawasiliano yanaweza kusimamishwa na kunaweza kuwa na idadi kubwa ya majeruhi yakiathiri uwezo wa watoa huduma wa kwanza kuwafikia watu wote mara moja na kwa haraka.

C. Saa 72 za kwanza ni muda wa kawaida kwa wahudumu wa kwanza wa kukabiliana na maafa na timu ya kukabiliana na matibabu kufika kwenye eneo la tukio na kuwa na muda wa kutosha wa kutathmini hali, kutambua hatua bora zaidi ya kuchukuwa na kisha kukabili tukio.

D. Ili kuokoa maisha, hatua zifuatazo zinapaswa kufanywa ndani ya masaa 72:

1) Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Menejimenti ya Maafa itaamsha Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura na kuitisha mkutano wa awali wa taarifa na tathmini. Aidha, itaandaa mfumo wa kutoa taarifa na ratiba ya kawaida ya mikutano.

2) Ofisi ya Waziri Mkuu- Idara ya Menejimenti ya Maafa itaanzisha Timu ya Kukabiliana na Maafa kwa Haraka. Uundaji wa timu hiyo utategemea na aina ya maafa yaliyotokea. Timu hiyo itajumuisha wataalam mbalimbali wa masuala ya kitaalam kama vile tathmini ya uharibifu, Usalama wa Chakula, Afya ya Umma, Ufuatiliaji wa magonjwa (Epidemiolojia), Maendeleo ya Jamii, Maji na Usafi wa Mazingira, Utawala na Ugavi pamoja na wataalam wa mawasiliano. Timu itatumwa mara moja wakati maafa makubwa yanapotokea.

3) Timu ya Kukabiliana na Maafa kwa Haraka itatembelea eneo lililoathiriwa na kufanya tathmini ya haraka na kuandaa taarifa ya awali ya maafa. Timu itatoa taarifa haraka iwezekanavyo kuhusu kiwango ambacho idadi ya watu imeathirika na taarifa kuhusu aina na ukubwa wa maafa. Aidha, Timu itabainisha ukubwa wa uharibifu, upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kukabiliana, na mahitaji ya haraka ya waathirika. Kutokana na taarifa ya tathmini, Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Menejimenti ya Maafa itatayarisha maombi kwa ajili ya aina maalum za usaidizi unaohitajika kama vile chakula, vifaa vya matibabu na inaweza kuomba kutengewa fedha za dharura.

4) Timu za utafutaji na uokoaji itaamshwa na kuelekea kwenye tukio ndani ya saa chache baada ya janga kubwa kama vile mafuriko, tetemeko la ardhi, dhoruba kali za kitropiki au tsunami kutokea.

5) Usalama unapaswa kushughulikiwa wakati wa saa za mwanzo za maafa makubwa. Matukio ya maafa hayasababishi kuvunjika kwa matumizi ya Sheria na taratibu, lakini raia karibu kila wakati huwa na wasiwasi kwamba hili litatokea. Kwa hivyo, lengo la kusimamia hali ya usalama ni kutoa ushahidi unaoonekana wazi kwamba sheria zitaendelea kutekelezwa, na pia kuzuia wananchi wasifike katika maeneo ambayo kuna hatari zinazoendelea zinazotishia afya na usalama wa umma.

6) Kuna uwezekano kwamba taarifa katika saa za mwanzo za maafa hazitapatikana wala hazitakuwa za kuaminika. Katika hatua hii changamoto kubwa ni kuhakikisha kuwa taarifa hizo ziko wazi na zinaakisi mahitaji ya dharura ya watu walioathirika. Mtaalamu wa mawasiliano atawajibika kukusanya taarifa na kuzisambaza kwa wakati na kwa ufanisi kwa kufuata taratibu zilizopo.

7) Taarifa kuhusu maafa zitapokelewa, kupangwa, kuchakatwa na kusambazwa kwa kufuata taratibu za mawasiliano za serikali.